**HOTUBA YA MHE. JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI WAKATI WA KUFUNGA MAFUNZO YA MAWAKILI WA SERIKALI YALIYOANDALIWA NA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KATIKA UKUMBI WA LUSH GARDEN, ARUSHA TAREHE 22 MEI, 2024**

**Mhe. Emmanuel Kawishe- Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania,**

**Mhe. Robert V. Makaramba - Jaji (Mst) Mahakama Kuu ya Tanzania,**

**Dkt. Boniphace Luhende - Wakili Mkuu wa Serikali,**

**Bi. Alice E. Mtulo – Naibu Wakili Mkuu wa Serikali,**

**Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,**

**Mawakili wa Serikali na Maafisa sheria mliopo,**

**Waandishi na Maafisa Habari,**

**Wageni Waalikwa,**

**Mabibi na Mabwana.**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!...................**

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

1. Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetukirimia uhai, uzima na afya na kutupa fursa ya kuiona siku hii ya leo. Tunamuomba baraka zake zisipungue maishani mwetu.
2. Pili, napenda kukushukuru Dkt. Boniphace N. Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Menejimenti ya Ofisi ya Wakili ya Wakili Mkuu wa Serikali na watumishi wote kwa kufanikisha mafunzo haya ya Mawakili. **Hongereni sana.** Pia nashukuru kwa hotuba zenu tangulizi ambazo zimenipatia muhtasari wa namna ratiba ya mafunzo ilivyotekelezwa**.**

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

3. Kwa kuwa jana tarehe 21.5.2024 Wakili mwenzetu, Bi. Lina Robert Msanga, mwenye Namba ya Usajili Na. 742 alifariki huko nchini India alikokuwa anaendelea kupata matibabu, napenda kutoa pole kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, Familia ya Msanga, Watumishi na Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambako ndiko marehemu alikuwa akifanya kazi, Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania, Mawakili wote wa Serikali na watumishi wote katika Ofisi zetu kwa msiba huu. Naomba sasa wote tusimame kwa dakika chache ili tumwombe Mungu aipumuzishe kwa amani Roho ya Wakili Lina Robert Msanga….Amina!

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

4. Nimeelezwa na Wakili Mkuu wa Serikali kuwa Naibu Waziri wetu wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb), alifungua mafunzo haya tarehe 20 Mei, 2024. Na mimi nimekabidhiwa jukumu la kufunga mafunzo haya ya Mawakili wa Serikali kwa mwaka 2024 siku hii ya leo. Ninashukuru sana kwa kupewa nafasi hii. **Asanteni sana.**

5. Nimefahamishwa kuwa Mafunzo haya ya mwaka 2024 yanayoratibiwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yamehusisha takribani washiriki wa Serikali ***mia*** tano kutoka Wizara mbali mbali, Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tanzania na Zanzibar, Taasisi za Serikali, Idara, Mashirika, kampuni mbalimbali za Serikali pamoja na Taasisi za kifedha ikiwemo benki mbalimbali nchini.

6. Ni furaha yangu kuwa kwa mara nyingine tena mmehakikisha kuwa mafunzo haya yana wawakilishi kutoka kwenye kila Wizara, idara, taasisi ya Serikali na kampuni ambazo Serikali ina hisa. Ninaomba ushirikishwaji huu uendelee na miaka ijayo tujipange kuongeza wigo ili kutoa mafunzo kwa Mawakili wengi zaidi.

7. Aidha, nimedokezwa kuwa mafunzo haya yamefadhiliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali. Naomba niungane na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuzishukuru taasisi zote zilizowezesha mafunzo haya kwa kuchangia kiasi cha fedha ili kuongeza nguvu ya kufanikisha mafunzo haya kwa ufanisi mkubwa. Tunatambua mchango mkubwa wa taasisi hizo kwenye mafunzo haya yanayolenga kulinda maslahi ya nchi kwa kupitia majukumu yanayotekelezwa na Mawakili wa Serikali.

8. Sambamba na hili, nichukue fursa hii kuzishukuru Taasisi zilizowaruhusu Mawakili wa Serikali kushiriki na kuhudhuria katika mafunzo haya maalumu. **Ninawapongeza sana kwa ushirikiano huu.**

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

9. Nimesikia kuwa lengo kuu la mafunzo haya ni kuwaongezea Mawakili wa Serikali maarifa na ujuzi zaidi katika maeneo mtambuka ambayo Mawakili hujishughulisha nayo ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwa weledi mkubwa zaidi. Lengo hili

lilizalisha kauli mbiu isemayo, "***Uendeshaji wa Mashauri ya Serikali; Wajibu na Majukumu ya Wakili wa Serikali".***

10. Naomba Mawakili wote tukumbuke kuwa tunawajibu kwa Serikali na Nchi kwa ujumla kwenye kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Hivyo, ni rai yangu kuwa kutokana na mafunzo haya, tumekumbushwa tena wajibu wetu kama mawakili wa serikali na kuelewa majukumu yetu. Hivyo natarajia tutatekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na weledi mkubwa.

**Ndugu washiriki wa mafunzo**

11. Nimefahamishwa kuwa katika kipindi cha siku tatu za mafunzo, mmejifunza masuala mbalimbali ya kisheria ikiwemo:

   i. *udhibiti ubora kwenye uendeshaji wa mashauri*;
   ii. taratibu za uendeshaji wa mashauri ya kinidhamu kwa watumishi wa umma;
   iii. *utatuzi wa migogoro inayohusisha Sekta ya Madini na Maliasili;*
   iv. *taratibu za uendeshaji wa mashauri ya usuluhishi wa kitaifa;*
   v. *taratibu za utatuzi wa migogoro chini ya mikataba ya uwekezaji;*
   vi. *usimamizi wa mikataba na utatuzi wa migogoro inayotokana na mikataba*;
   vii. *taratibu za uendeshaji wa mashauri ya Mahakama za Rufani kwa kuzingatia mabadiliko ya kanuni za Mahakama ya Rufani za Mwaka 2024*,
   viii. *masuala ya kuzingatia katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali;* na

ix. *mabadiliko ya sheria za uchaguzi*.

Nawapongeza sana wakufunzi wetu kwa kujitoa kwao na kufanya maandalizi ya kutosha. Nimefanya kazi na wengi wao na ninaelewa michango ya Mhe. Prof. Kabudi (Mb), Mhe. Jaji Makaramba, Mhe. Jaji Kawishe,na Prof. Kennedy Gastorn pamoja na wengine, katika maboresho makubwa yaliyofanyika katika Sekta ya Sheria hususan Mahakamani, OMMS, OTM, OWMS, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi n.k. Tutaendelea sana kuwatumia wakufunzi hawa na wengine wengi tulio nao ndani na nje ya nchi.

12. Mada hizi na nyingine zilizotolewa na wakufunzi wabobevu zimelenga kuwanoa ili kuwafanya kuwa Mawakili bora katika kuunga mkono jitihada za Serikali yetu ya Awamu ya Sita ambayo inafanya juhudi za makusudi kuvutia wawekezaji ili kukuza uchumi wa nchi yetu. Kama tunavyofahamu ili wawekezaji wavutiwe kuja ni lazima tuwe na mifumo imara na thabiti ya sheria. Hivyo, ni rai yetu sisi kama Mawakili tuliokabidhiwa jukumu la kusimamia na kutekeleza masuala ya sheria kwenye taasisi zetu tuwe na elimu ya kutosha kuhusu masuala mbalimbali ya sheria ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima na kudumisha imani ya wananchi na wawekezaji pale inapojitokeza migogoro.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

13. Pamoja na mada nyingi mlizofundishwa ninafahamu pia mlifundishwa masuala ya udhibiti ubora na usimamizi wa mashauri. Ni muhimu

kwetu Mawakili sio tu kuendesha mashauri bali pia kuendesha na kusimamia uendeshaji wa mashauri kwa ubora na viwango vya hali ya juu. **Sitegemei kuona Wakili wa Serikali akiendesha shauri bila kujali kuwa anawakilisha Serikali, yeye anasimama kwa niaba ya Serikali na ana jukumu la kulinda rasilimali zetu**. Hivyo, tukitambua hayo natumaini mafunzo haya yametupa mwangaza wa viwango vya kuzingatia kama Mawakili wa Serikali tunapotekeleza majukumu yetu.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

14. Mkiwa Mawakili wa Serikali mnaoendesha na kusimamia mashauri ya Serikali mlipata wasaa wa kupitishwa kwenye mada inayohusu utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, usimamizi wa mikataba na utatuzi wa migogoro inayotokana na mikataba pamoja na utaratibu wa utatuzi wa migogoro chini ya mikataba ya uwekezaji. Dunia sasa inabadilika na kukaribisha utatuzi wa migogoro kwa haraka zaidi kwa njia mbadala za utatuzi wa migogoro ikiwemo njia ya usuluhishi. Hivyo ni muhimu kupata ujuzi kuhusu njia hizo na namna ya kushughulikia migogoro inayotokana na mikataba ya Serikali na wadau wengine pamoja na mikataba ya nchi yetu na nchi nyingine.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

**15.** Sambamba na mada hiyo, pia mlifundishwa kuhusu namna ya **kuendesha mashauri ya Serikali na wajibu wa Mawakili wa Serikali katika utoaji wa taarifa za mashauri**. Nilieleza mwaka jana kwenye uzinduzi wa Chama cha Mawakili wa Serikali kuwa Mawakili wote wanatakiwa kuwasilisha taarifa zao za mashauri kwa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Naomba nisisitize kuwa suala hili ni muhimu sana na kila Mkuu wa Idara au Kitengo cha Sheria ahakikishe kuwa agizo hili linatekelezwa. **Pia, tusisahau kuwasilisha taarifa za uendeshaji wa mashauri kwa Wakili Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa nyenzo *(instrument)* ya kuendesha mashauri kwa niaba ya Serikali.** Tunao wajibu wa kutekeleza masharti ya Hati hizo hizo **ambazo nilielekeza zitolewe kwa Mawakili wote wenye sifa kwa mujibu wa Daftari la Usajili la Mawakili wa Serikali ili kumwezesha Wakili Mkuu wa Serikali kuwapangia kazi kulingana na uwezo wa kila Wakili na aina ya kesi anayoweza kumudu kuiendesha mbele ya vyombo vya kutoa maamuzi. Naomba nisisitize hili tuliwekee mkazo wa kutosha.**

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

**16.** Nawapongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kwa kuona umuhimu wa kutoa mafunzo kuhusu mabadiliko ya sheria ya uchaguzi tukitambua wazi kuwa mwaka huu tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mwaka ujao wa 2025 kutakuwa na uchaguzi mkuu. Hivyo, ni vyema tukajiandaa vizuri kwenye suala hili ili tuweze kuishauri vyema Serikali kuhusu masuala ya uchaguzi na pale kutakapokuwa na mashauri yanayohusu uchaguzi tuweze kuiwakilisha Serikali kwa weledi mkubwa kwenye mashauri hayo. **Naomba mara tu Kanuni za Uchaguzi wa Serikali wa Mitaa zitakapotoka hivi karibuni OWMS ishirikiane na Mawakili wa Serikali walio TAMISEMI kuweka mazingira wezeshi kuhakikisha zinatumika kwa mujibu wa sheria.**

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

17. Naomba niwapongeze tena Mawakili wa Serikali kwa kazi nzuri mnazoendelea kuzifanya katika taasisi zenu. Nawasihi muongeze juhudi, kujituma, msiache kuuliza pale ambapo mmekwama na kudumisha ushirikishwaji kwenye kila hatua mnayochukua ili twende pamoja.

    Ni rai yangu kuwa kupitia mafunzo haya pamoja na mambo mengine mengi niliyoyaeleza hapo juu, baada ya mafunzo haya, Ofisi yangu na Serikali kwa ujumla,w inatarajia mambo yafuatayo kutoka kwenu:-

    i. Mtawashauri vyema waajiri katika kushughulikia masuala ya ajira na nidhamu ili kuiepusha Serikali kupata hasara na kulipa fidia kwa watumishi wanaoajiriwa na kusimamishwa au kufukuzwa bila kuzingatia sheria, taratibu na miongozo iliyopo;

    ii. Mtafanya kazi kwa kuzingatia miongozo mbalimbali iliyopo ya Mawakili wa Serikali;

    iii. Mtajikita zaidi katika kuhakikisha migogoro inapojitokeza inashughulikiwa kwa haraka kwa njia za usuluhishi au majadiliano ili kupunguza uzalishaji wa kesi;

    iv. Mtaendelea kuzishauri vyema taasisi zenu katika kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya kusimamia utekelezaji wa mikataba ili kuongeza tija na ufanisi Serikalini;

    v. Mtakuwa sehemu ya kuisaidia Serikali katika kuvutia wawekezaji kupitia maarifa mliyopatiwa kuhusu sheria zetu zinazosimamia uwekezaji;

vi. Mtawashauri vyema Viongozi kuhusu masuala yote ya kuzingatia katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na baadaye Uchaguzi Mkuu;

vii. Mnahimizwa kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa mashauri ya madai na usuluhishi kabla, wakati na baada ya kuendesha mashauri hayo **na kutoa ushirikiano kwa kaguzi zinazotarajiwa kufanyika kuanzia mwezi Julai, 2024;**

viii. Kila mmoja ataendelea kubainisha maeneo anayohitaji kujengewa uwezo ili kumwezesha kutekeleza majukumu yake;

ix. Kuendelea kufanya tafiti katika maeneo mapya na ya kimkakati na kutoa matokeo ya tafiti hizo kwa wakati;na

x. Kuwa tayari kufanya kazi zingine mtakazopangiwa na MMS, WMS na DPP kwa mujibu wa Sheria. Wakili wa Serikali ni Wakili wa Umma ndiyo maana hapaswi kuwa na mipaka finyu katika maeneo ya kutekeleza majukumu yake kwa Taifa lake.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**

18. Kama mnavyofahamu, hii ni mara ya tano kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuandaa mafunzo ya aina hii ambayo yanahusisha Mawakili wa Serikali kutoka Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali na mafunzo haya ni endelevu, hivyo, michango yenu ya namna ya kuboresha mafunzo haya yanakaribishwa wakati wowote kupitia barua pepe ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ***info@osg.go.tz.***

19. Kipekee kabisa napenda kuishukuru tena Serikali kwa kuridhia matumizi ya fedha kwa mafunzo haya maalumu kwa Mawakili wa Serikali ambayo yameratibiwa vyema na Kamati ya Maandalizi ya Mafunzo chini ya usimamizi wa Menejimenti ya OWMS.

20. Kwa heshima na taadhima sasa ninayo furaha kutamka rasmi kuwa mafunzo haya yamefungwa rasmi na nawatakia kila la kheri kwa wale wote mtakaosafiri kuelekea katika vituo vyenu vya kazi.

**Mungu Ibariki Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali!**

**Mungu Ibariki Tanzania!**

**Asante sana kwa kunisikiliza!**



Mhe. Jaji Dkt.Eliezer Mbuki Feleshi
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**